


# Taarifa ya
# Ofisi Ya Katibu Mkuu

Pr. Onesmo M. Daniel

## UTANGULIZI.


Awali ya yote, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu aliyetusaidia kuifikia siku hii ya leo ya mkutano mkuu wa Kanisa la South Nyanza Conference. Natoa shukrani zangu kwa maofisa wa Union ya Kaskazini mwa Tanzania, Wajumbe wa Kamati Kuu Tendaji ya SNC, Wachungaji wenzangu, Viongozi waliotutangulia, Watendakazi wa makao makuu ya SNC, Watumishi katika Taasisi zote za Conference, na kwa washiriki wote wa SNC kwa ushirikiano wao, kazi njema zilizotendwa kupitia mshiriki mmoja mmoja na kwa Kanisa kwa ujumla katika muhula huu wa uongozi.

South Nyanza Conference ndani ya kipindi hiki tangu Sept 2022 hadi Juni 2025 imeweza kufanya kazi nyingi kupitia makanisa yake na katika kueneza injili, kazi iliyopelekea ongezeko la washiriki, mitaa, makanisa, makundi, watumishi na hatimaye kuzaliwa kwa Field mpya ya Simiyu River Field, Bwana Atukuzwe.


## ENEO LA UTUME

Katika kipindi cha Septemba 2022 hadi Mei 2025 South Nyanza Conference imeendelea kufanya shughuli za Utume na malezi ya waumini katika eneo la kiutawala la mikoa ya Simiyu na Mwanza *(ukiondoa Wilaya za Ukerewe, Buchosa na Sengerema)*. Makao Makuu ya Conference yako eneo la Pasiansi katika kata ya Kawekamo, Wilayani Ilemela, mkoa wa Mwanza. Katika kipindi hiki Conference ilijulikana kwa kuwa na Kanda nne za kijimbo ambazo zilikuwa ni Bariadi, Meatu, Maswa na Mwanza.

*Picha 1: Eneo la Utume la South Nyanza Conference kwa Kipindi cha Septemba 2022 - Mei 2025.*



Mwezi Mei 2025 Field ya Simiyu River ilipangwa rasmi na kufanya eneo la utume la South Nyanza Conference kubakia katika eneo la kiutawala la Wilaya za Ilemela, Nyamagana, Magu, Misungwi na Kwimba ndani ya Mkoa wa Mwanza.




*Picha 2: Eneo la Utume la South Nyanza Conference baada ya Kutengwa kwa Simiyu River Field Mei 2025.*

## UKUAJI WA KANISA

Kwa rehema za Bwana na kupitia mikakakati mbalimbali ya kiutume kipindi hiki Kanisa katika South Nyanza Conference limeshuhudia ukuaji wa aina yake ambapo kumekuwepo ongezeko la 26.3% katika idadi ya washiriki katika SNC jambo ambalo ni ushuhuda wa Nguvu ya Mungu itendayo kazi katika Kanisa lake.

| MWAKA | MITAA | MAKANISA | MAKUNDI | WASHIRIKI |
|---|---|---|---|---|
| Sept 2022 | 78 | 647 | 325 | 168,252 |
| June 2025 | 97 | 763 | 329 | 212,530 |
| **Ongezeko** | **19** | **116** | **4** | **44,278** |
| **Asilimia Ong** | **24.4%** | **17.9%** | **1.2%** | **26.3%** |

*Takwimu za vituo vya utume na idadi ya washiriki 2022 na 2025*

| | MITAA | MAKANISA | MAKUNDI | WASHIRIKI |
|---|---|---|---|---|
| Des 2022 | 78 | 651 | 336 | 170,313 |
| Des 2023 | 95 | 687 | 349 | 187,175 |
| Des 2024 | 96 | 739 | 338 | 203,341 |
| Jun 2025 | 97 | 763 | 329 | 212,530 |

### MALEZI NA MATUNZO YA WASHIRIKI


Tunamshukuru Bwana kwa namna ambavyo ameliongoza Kanisa lake katika South Nyanza Conference kukua sana kwenye muhula huu. Kwa uongozi wa Roho Mtakatifu washiriki wetu wakishirikiana na wachungaji wao wamekua na bidii sana katika kufanya Uinjilisti, kubatiza watu wengi na pia kutunza wale wanaobatizwa.



*Picha 3: Washiriki wa Kanisa Mahalia wakiwa na Wabatizwa Wapya (Walio katikati) na Vyeti vya Ushiriki wao Katika Mahubiri.*

### *Ongezeko la Waumini Kwa Robo Sept 2022 – Juni 2025*


Kwa mujibu wa taarifa za washiriki ambazo zimekua zikikusanywa kila Robo kwa muhula huu zimeonesha ongezeko kama ifuatavyo; Mwaka 2022 Robo ya 3 (**168252**), Mwaka 2022 Robo ya 4 (**170313**), Mwaka 2023 Robo ya 1 (**171783**), Mwaka 2023 Robo ya 2 (**178827**), Mwaka 2023 Robo ya 3 (**186304**), Mwaka 2023 Robo ya 4 (**187175**), Mwaka 2024 Robo ya 1 (**187345**), Mwaka 2024 Robo ya 2 (**196300**), Mwaka 2024 Robo ya 3 (**201792**), Mwaka 2024 Robo ya 4 (**203341**), Mwaka 2025 Robo ya 1 (**205866**), na Mwaka 2025 Robo ya 3 (**212530**).




*Jedwali 1: Ongezeko la Waumini kwa Kila Robo Kuanzia Septemba 2022 hadi Juni 2025*

### *Waumini Walioongezeka Katika Muhula*


Katika kipindi cha kuanzia Septemba 2022 hadi Juni 2025 washiriki takribani 59084 wameingizwa katika vitabu vyetu vya ushirika kupitia njia mbalimbali kama; Ubatizo kwa Waumini Wapya (54197), Ubatizo Waumini Waliorejeshwa (1709), Waliopokelewa kwa Barua kutoka Makanisa Mengine ya Kiadventista (3134), Kukiri Imani (29), na Marekebisho (15).




*Jedwali 2: Mchanganuo wa Washiriki Walioingizwa Katika Vitabu vya Ushirika vya Makanisa ya South Nyanza Conference kwa Kipindi cha Septemba 2022 hadi Juni 2025.*

### *Waumini Waliopungua Katika Muhula.*

Jumla ya majina 10,533 yaliondolewa katika vitabu vyao ushirika ambapo 77.8% yalihamishwa kwenda kwenye makanisa mengine ndani na nje ya Conference yetu, 11.2% kwa kufutwa ushirika, kwa kutojulikana walipo 0.6% na 10.4% kwa kupoteza maisha.




*Jedwali 3: Mchanganuo wa Washiriki Walioondolewa Katika Vitabu vya Ushirika vya Makanisa ya South Nyanza Conference kwa Kipindi cha Septemba 2022 hadi Juni 2025.*

## Muhtasari wa Mfumo wa ACMS.

Kwa kushirikiana na Idara ya mawasiliano kupitia kitengo cha TEHAMA tumeendelea kutoa elimu ya matumizi ya mfumo wa ACMS kupitia semina zilizofanyika katika Kanda, Mitaa na Makanisa ambapo hadi kufikia Juni 2025 washiriki 178000 walikua wamekwisha kuingizwa katika mfumo.



*Picha 4: Katibu Mkuu Pr. Onesmo akiwa katika moja ya semina za ACMS iliyofanyika Mabatini.*

## Kutekeleza Mkakati wa Kulea, Kutunza na Kurejesha Washiriki

- Kupunguza ukubwa wa mitaa kwa kuikata ili kusogeza huduma kwa washiriki
- Kufanya uchambuzi yakinifu wa washiriki kwa kila Kanisa ili kujua idadi halisi ya washiriki wa Kanisa.
- Kutoa Semina za kutosha za namna ya kuratibu washiriki kwa makarani wa makanisa yote.
- Kutoa Semina za malezi na matunzo ya washiriki kwa mitaa yote ndani ya Conference
- Semina za urejeshwaji kwa wachungaji, wazee wa makanisa, viongozi wa makanisa na washiriki wote
- Kila mchungaji, wazee wa makanisa, washiriki kuhusika katika kuwarejesha watu
- Kila robo kutakuwa na siku ya kurejesha watu kwa Jimbo zima.

## Changamoto katika Malezi, Matunzo na Urejeshaji wa Washiriki

- Bado kuna mitaa mingi inayohitaji kukatwa ili kusogeza huduma za kichungaji kwa washiriki.

- Makarani wa Kanisa kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya uratibu wa majina ya washiriki.
- Uhamaji wa washiriki unaosababishwa na utafutaji wa maisha (kilimo, ufugaji, biashara n.k) unatufanya tupoteze washiriki wengi.
- Batizo zinazolenga kupata idadi kubwa ya wabatizwa na si washiriki wanaodumu kanisani (quantitative vs qualitative church growth).
- Makanisa kutoona umuhimu wa kupitia orodha ya majina ya washiriki katika kitabu cha ushirika mara kwa mara ili kujua nani hayupo na kuwatafuta kabla hawajasahaulika na hatimaye kupotea.
- Eneo dogo la ofisi yetu kwa sasa.

## UWIANO WA WASHIRIKI KWA WAKAZI

Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 eneo la utume linalohudumiwa na South Nyanza Conference lina jumla ya wakazi wapatao 4,614,029 na hivyo kufanya uwiano wa mshiriki kwa wakazi kuwa mshiriki mmoja (1) kwa kila wakazi ishirini na mbili (22). Hii inatupatia picha ya kuwa japo kazi iliyofanyika ni kubwa, bado kuna kazi kubwa zaidi ya kuhakikisha tunatimiza utume wetu wa kuwafanya "wote kuwa wanafunzi".

| MKOA | IDADI MITAA | IDADI MAKANISA | IDADI MAKUNDI | IDADI WASHIRIKI | WAKAZI | UWIANO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MWANZA | 45 | 291 | 105 | 90,094 | 2,473,532 | 1:27 |
| SIMIYU | 52 | 472 | 224 | 122,436 | 2,140,497 | 1:17 |
| **JUMLA** | **97** | **763** | **329** | **212,530** | **4,614,029** | **1:22** |

## WATUMISHI NA RASILIMALI WATU.

Ukuaji huo wa kazi ulioshuhudiwa katika kipindi hiki pia ulipelekea ongezeko la watenda kazi ili kukidhi mahitaji ya kazi katika maeneo yetu ambapo limekuwepo ongezeko la jumla ya watumishi 27 toka kwa watumishi 372 na kufanya jumla ya watumishi wanaolihudumia Kanisa katika kada mbalimbali kufikia 399.

| NA | TAASISI | MWAKA 2022 | MWAKA 2024 |
|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu | 124 | 155 |
| 2 | Bupandagila Adventist High School | 53 | 32 |
| 3 | Nyanza Adventist Secondary School | 48 | 39 |
| 4 | Pasiansi SDA Hospital | 71 | 86 |
| 5 | Ngulyati Adventist Secondary School | 21 | 20 |
| 6 | Wainjilisti wa Vitabu Cheti cha Pili na Tatu | 55 | 43 |
| 7 | Bupandagila Adventist Primary School | - | 24 |
| | ***Jumla kuu*** | ***372*** | ***399*** |

## Mchanganuo wa Kada na Elimu za Watumishi Katika SNC

**HOSPITALI YA SDA PASIANSI HOSPITAL**

| KUNDI | Uz | Sh | St | Ch | V | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Madaktari Bingwa | 1 | | | | | 1 |
| Waganga | - | 9 | 2 | - | - | 11 |
| Katibu wa Afya | - | 1 | - | - | - | 1 |
| Wauguzi | - | 1 | 8 | 7 | - | 16 |
| Wasaidizi wa Afya | - | - | - | 12 | - | 12 |
| Maabara | - | 4 | 2 | 0 | - | 6 |
| Madawa | - | 1 | 3 | 1 | - | 5 |
| Mionzi | - | - | 2 | 1 | - | 3 |
| Wahasibu | - | 3 | 2 | 1 | - | 6 |
| Usafi | - | - | - | 2 | 4 | 6 |
| Mapokezi | - | - | 2 | 1 | 2 | 5 |
| Walinzi | - | - | - | 3 | 1 | 4 |
| IT | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Fundi Sanifu Vifaa Tiba | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Wengineo | - | 6 | 1 | 1 | - | 8 |
| **Jumla** | **1** | **25** | **24** | **29** | **7** | **86** |

**SHULE YA MSINGI YA BUPANDAGILA ADVENTIST.**

| Makundi | Uz | Sh | St | Ch | V | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | - | 2 | 5 | 4 | - | 11 |
| Wahasibu | 1 | - | - | 1 | - | 2 |
| Wengineo | - | - | 2 | 1 | - | 11 |
| ***Jumla*** | ***1*** | ***14*** | ***7*** | ***6*** | ***-*** | ***24*** |

**SHULE YA SEKONDARI YA NYANZA ADVENTIST**

| Makundi | Uz | Sh | St | Ch | V | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | 4 | 21 | 1 | - | - | 26 |
| Wahasibu | - | 4 | - | - | - | 4 |
| Wauguzi | - | - | - | 1 | - | 1 |
| Wengineo | - | - | 1 | 7 | - | 8 |
| ***Jumla*** | ***4*** | ***24*** | ***2*** | ***8*** | ***0*** | ***39*** |

**SHULE YA SEKONDARI BUPANDAGILA ADVENTIST**

| Makundi | Uz | Sh | St | Ch | V | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | - | 14 | 2 | - | - | 16 |
| Wahasibu | - | 1 | 1 | - | - | 2 |
| Mganga | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Maabara | - | - | - | 1 | - | 1 |
| Wauguzi | - | - | 2 | - | - | 2 |
| IT | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Wengineo | - | - | 1 | 1 | 7 | 9 |
| ***Jumla*** | ***-*** | ***15*** | ***8*** | ***2*** | ***7*** | ***32*** |

**SHULE YA SEKONDARI NGULYATI**

| Makundi | Uz | Sh | St | Ch | V | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Walimu | - | 10 | 2 | - | - | 12 |
| Wahasibu | 1 | - | 1 | - | - | 2 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wengineo | - | 1 | - | 1 | 4 | 6 |
| ***Jumla*** | ***1*** | ***11*** | ***3*** | ***1*** | ***4*** | ***20*** |

**WAINJILISTI WA VITABU**

| Mwaka | Cheti cha 3 | Cheti cha 2 | Cheti cha 1 | Wa muda | Wapya | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2023 | 29 | 26 | 194 | 49 | | 298 |
| 2024 | 28 | 25 | 268 | 36 | | 357 |
| 2025 | 26 | 17 | 181 | 36 | 7 | 267 |

**WATENDAKAZI MAKAO MAKUU**

| Makundi | S7 | Sk | Ch | St | StJ | Sh | Uz | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wachungaji | 3 | 16 | 10 | 5 | 0 | 63 | 9 | |
| Fani tofauti na uchungaji | | | | 2 | 1 | 5 | | 114 |
| Wahasibu | - | - | - | - | 2 | 11 | 2 | 15 |
| Walimu | - | - | - | - | - | - | 1 | 1 |
| K. Wahitasi | - | - | - | 4 | - | 3 | - | 7 |
| Teknohama | - | - | - | 1 | - | 1 | - | 2 |
| Habari | - | - | - | 1 | - | - | - | 1 |
| APD | 1 | - | - | - | - | 2 | - | 3 |
| Dereva | - | - | 1 | - | - | - | - | 1 |
| Meneja Miliki | - | - | - | - | 1 | - | - | 1 |
| Meneja Miradi | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mazingira | 4 | - | - | 1 | - | - | - | 5 |
| Walinzi | 3 | 2 | - | - | - | - | - | 5 |
| ***Jumla*** | ***11*** | ***18*** | ***11*** | ***14*** | ***4*** | ***85*** | ***12*** | ***155*** |

Katika watumishi hawa wapo baadhi ambao wanaendelea na masomo yao ambapo katika Idara ya mawasiliano mtumishi mmoja anachukua Master's Degree of Cyber Security and Digital Forensic, Kitengo cha Tehama mtumishi mmoja anachukua Bachelor of Science in ICT, Idara ya Sekretariet mtumishi mmoja anachukua Master's Degree of Business Administration in Human Resource, Idara ya Uwakili na Majengo mtumishi mmoja anachukua Bachelor of Science in Environmental Science na Mtumishi mmoja wa Kitengo cha Sekretariet amemaliza masomo yake ya Bachelor Degree of Business Administration and Secretarial Science. Tunawatia moyo wengine wajiendeleze wasonge mbele.

**WACHUNGAJI**

| Makundi | Ofisini | Mitaani | Taasisi | Wastaafu | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Waliowekewa Mikono | 8 | 33 | 3 | 10 | 45 |
| Hawajawekewa Mikono | 1 | 67 | 2 | - | 69 |
| ***Jumla*** | ***9*** | ***99*** | ***5*** | ***10*** | ***114*** |

Timu hii ya wachungaji kazini, inaungana na wachungaji wastaafu 10 wenye mikono ambao ni mbaraka mkubwa kwa kazi. Wachungaji hao wastaafu ni Mch. Isaack Maiga, Mch. Joseph Bulengela, Mch. Methusela Masuke, Mch. Erasto Mitanda, Mch. Fredy Kuleng'wa, Mch. Lameck Bulugu, Mch. Lucas Makondo, Mch. Yusuph Masunga, Mch. Ibrahim Alex Juma na Mch. William Busee. Hawa wanashiriki katika kulisha siku za Ibada, mikutano ya makambi,

Ubatizo, Ndoa, mahubiri ya hadhara na huduma nyingine nyingi za Kanisa na jamii.

Kwa masikitiko makubwa tulipata msiba wa Mchungaji Sengiyumva Shaltiel Siniga aliyefariki tarehe 25/02/2024 kwa ajali ya kugongwa na gari alipokuwa anatoka kutembelea washiriki mtaani kwake na Mchungaji Joseph Juma Apollo aliyefariki tarehe 19/02/2025 alipatwa na umauti katika Hospitali ya Rufaa Bugando alipokuwa akipatiwa matibabu, alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya kisukari.

Tuzidi kuwaombea wachungaji wetu mmoja mmoja ambao wanachangamoto kubwa za kiafya.

Tangu Septemba 2022 hadi Juni 2025 kumekuwepo na matukio ya uwekaji mikono wachungaji matatu ambapo jumla ya wachungaji 8 wamewekewa mikono. Pia katika kipindi hiki wameajiriwa wachungaji wapya 9. Wachungaji masomoni ni 18, wanaosoma wakiwa kazini ni 15, mmoja anasoma akiwa katika likizo ya bila malipo. Wachungaji wawili, Lameck Yohana, Shabani Kwilasa wako nje ya utumishi wa kichungaji (leave of absence).

## SHEREHE ZA MIAKA 150 YA UTUME

Kuanzia tarehe 22 hadi 24 Agosti 2024, Washiriki, Viongozi na Watendakazi wa South Nyanza Conference tulikusanyika katika Shule ya Sekondari Bupadagila ambapo tulikuwa na kumbukizi ya miaka 150 ya utume ulimwenguni na miaka 112 ya utume katika South Nyanza Conference. Sherehe hizi za utume zilizosimamiwa na Mch. Mark Walwa Malekana, Mwenyekiti wa NTUC.

Katika sherehe hizo zilifanyika shughuli mbalimbali kama kutazama Makala za historia ya utume SNC, kupanda miti, kuweka jiwe la msingi na masomo ya biblia.



*Picha 5: Wafanyakazi wa Makao Makuu ya SNC wakiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa NTUC Pr. Mark Malekana wakati wa Maadhimisho ya miaka 150 ya utume ulimwenguni.*

## KUANDAA WATUMISHI WA KANISA

Ofisi ya South Nyanza Conference imeendelea kutoa nafasi ya pekee kwa wachungaji, wahasibu, walimu na Teknohama, Makatibu wahitasi na watu wa mazingira kutoka vyuo mbalimbali ili kufanya mazoezi ya kile walichojifunza Vyuoni. Tendo hili limekuwa mbaraka mkubwa kwa watumishi waliokubali kufanya kazi na timu hizi.

Tumepokea wachungaji kwa ajili ya mazoezi kutoka chuo kikuu cha Arusha na Bugema. Lakini pia tumepata wanachuo wa kutoka VETA na pia vyuo vya Dodoma, SAUT, Chuo cha Mipango, Bugando na Vyuo mbalimbali vya Elimu, Teknohama, Uhasibu nk



*Picha 6: Katibu Mkuu Pr. Onesmo Daniel akikabidhi vyeti vya shukrani wanafunzi wawili waliofanya mafunzo kwa vitendo katika ofisi za makao makuu ya SNC.*

## KUSIMAMIA SUALA LA KUBADILI TASWIRA (IMAGE CHANGE)

Kubadili taswira (Image change) imekuwa ni mojawapo ya mambo yaliyokuwa katika misukumo ya kipindi hiki cha miaka mitatu kutoka ngazi ya General Conference. Lengo hasa likiwa ni kubadili mitazamo ya mshiriki mmoja mmoja na Kanisa kwa ujumla katika masuala yahusuyo miundombinu. Majengo yetu na miundombinu yote ya Kanisa kwa ujumla iliyoboreshwa vizuri yanaweza kutumika kama vyombo vya uinjilisti pale yanapoonekana kukidhi matarajio ya watu wa kizazi hiki kinachobadilika kwa kasi kubwa. Hii inakuwa tofauti na dhana ya kipindi kilichopita wakati majengo mengi ya makanisa yalipoonekana kuwa duni sana, washiriki wakidai kuwa duniani si mahali petu pa kudumu, tunasafiri, kitambo kidogo tutakuwa Mbinguni.

Katika kutekeleza jukumu hili tumetoa Semina kwa wachungaji na wazee wa Kanisa tukisisitiza umuhimu wa kujenga majengo mazuri ya Kanisa yanayomwakilisha vizuri Mungu pamoja na Kanisa lake katika jamii hii na tumetiwa moyo na mwitikio mkubwa uliopo katika kulitekeleza suala hili.

Kuna mwamko mkubwa sana katika makanisa. Mengi yamehamasika na yameamua kuacha majengo ya zamani yaliyochoka na kuanzisha majengo mapya yenye hadhi, na makanisa mengine mengi yana mpango huo pia.

Sambamba na ujenzi wa makanisa kuna mwitikio mwingine mkubwa wa kujenga nyumba za wachungaji ili kukuza heshima ya watumishi hawa na kupunguza gharama kubwa ya kupanga nyumba. Mitaa mingi imehamasika ambapo hadi sasa nyumba 49 zinatumika (15-SNC na 34–SRF)

## SHUKRANI

Nichukue fursa hii kumshukuru Mungu kuniwezesha kumtumikia katika Ofisi hii kwa kipindi hiki kinachomalizika, Jina lake na litukuzwe. Ninawashukuru Maofisa wenzangu ambao tumefanya nao kazi kwa ushirikiano mkubwa, pia viongozi wenzangu wa Idara ya Sekretariet niliopokea kijiti kwao.

Wajumbe wote wa Kamati Kuu ya Conference, wakurugenzi wa Idara zote katika Conference, watumishi wote wa ofisi ya Conference, Wakuu wa Taasisi zetu zote na Wachungaji wa mitaa. Kwa kila walichofanya kuhakikisha shughuli za Conference hii kwa kipindi hiki zinatekelezwa. Ninawashukuru viongozi wa makanisa mahalia, Makatibu wenzangu wa makanisa mahalia, wakuu wa Idara makanisani pamoja na waumini wote wa Conference hii kwa mshikamano mkubwa uliojidhihirisha katika kusukuma kwa pamoja kazi ya Mungu.

Asanteni kwa kuisikiliza kazi mliyoifanya nasi tukaipokea na kuijumlisha na kuisoma kwenu, asanteni kwa kunisikiliza, Nami nawasilisha. ASANTENI NA BWANA AINULIWE JUU, AMINA.

Neema ya Bwana Yesu Kristo na Ushirika wa Roho Mtakatifu vidumu kuwa pamoja nasi daima.